



REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

THIRD ASSEMBLY-SECOND SESSION

THE HANSARD

Tuesday, 19th March 2024

*The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 9:30 a.m.*

[The Speaker (Hon. Mwambire) in the Chair]

PRAYER

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

MCAS CONSULTATIVE MEETING WITH THE GOVERNOR

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Members, I have a Communication to share with you. For those Chairpersons and Vice-Chairpersons of all Committees, please when you are planning your work programme do not plan for Thursday this week maybe Friday onwards because the Governor intends to have a consultative meeting with you on a number of issues that are of great county concern. So, I will not approve any meeting on Thursday because of that. It is you Members who came to my Office with several issues you wanted to be looked into and I shared them with the Governor, and he asked to meet you on Thursday.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

MOTION**ADOPTION OF THE REPORT OF THE ICT AND RESEARCH COMMITTEE ON THE STATUS OF THE ICT CENTRES IN KILIFI COUNTY**

Hon. (Ms.) Faith: Thank you, Mr. Speaker. I want to move a Motion: -

THAT, This House adopts the Report of the ICT and Research Committee on the status of the ICT centres in Kilifi County laid on the Table of this House on Tuesday, 12th March 2024.

I call hon. Birya to second the Motion and I will give my response later.

Hon. Birya: Thank you, Mr. Speaker, I rise to second the Motion but before I sit, I would like to request that I make my submissions. Based on the recommendations of this Report, there is a need for more allocations to equip the VTC (Vocational Training College), and ICT (Information Communication and Technology) labs so that they can act as information centres to benefit the communities of their catchment. Thank you for this opportunity.

(Question proposed)

Hon. (Ms.) Sidi: Thank you, Mr. Speaker. I rise to support this Motion with a few observations. When we went round the VCT centres, we realized that not all the centres have computers, and we know very well that we are moving from paper to paperless. Our people on the ground need to be trained, educated and have knowledge about these gadgets. My humble request to the Department is they need to take this ICT programme very seriously to ensure that the centres that have these computers are serviced and have enough internet. We visited many centres, yes, they have computers, machines are there but they do not have internet. The internet came for only one month and the programme ended.

Secondly, we have VTCs that do not have machines and we have many students in those centres. I am sure this county can purchase machines for our students to learn. My request to the Department is to budget for these computers and internet and maintenance of these machines. Thank you. I rise to support.

The Speaker (Hon.Mwambire): Hon. Ngirani.

Hon. Ngirani: Thank you, Mr. Speaker. I rise to support this Report with a few observations that were made by the ICT Committee. When they went around the county inspecting the VTCs that we have, Mr. Speaker, from the observations and recommendations by the Committee, there is a big need for the Department of ICT to invest fully in ICT.

Mr. Speaker, we are in a century where Information and Communication technology are paramount, and it is because it has many advantages that suit our people in this sector. There is an increase in productivity and the creation of job opportunities through online job opportunities. We also have online sales, so from the Report, the ICT Department of Kilifi County is poorly implementing its objectives when it comes to ICT.

If I take an example of my VTC in Ganze, we only have two computers and the two were borrowed from Jaribuni VTC and one from Vitengeni VTC. This means the ICT Department has not contributed any computers to Ganze VTC. Mr. Speaker, we only have one instructor of ICT in Ganze VTC, and that one instructor was employed by the Board not even the county. We only have one employer from the County Government working as the Manager of Ganze VTC. There

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

is no classroom in Ganze VTC. The Office of the Manager is used as a classroom for learning ICT.

With those remarks, there is a need for the ICT Department to invest heavily in Information and Communication Technology in our VTCs. There is also a promise for an internet connection (WIFI) at Ganze Health Centre. That has not yet been done. We want the CECM (County Executive Committee Member) in charge of this Department to speed up the connectivity of the internet not only in Ganze but also to areas that were earmarked. With those few remarks, I support the Report and the recommendations. Thank you.

The Speaker (Hon.Mwambire): Hon. Brown.

Hon. Brown: Wacha kwanza nishukuru Maulana kwa afya ambayo ametupa na kuturudisha kazini. Bw. Spika, naunga mkono Ripoti hii ambayo mimi ni mmoja wa wanakamati na tulifanya kwa undani sana na utafiti. Kwangu mimi ningependa kupeana vidokezo kadhaa. Kuna sehemu kumi na tano ambazo ziliwekelewa ukuzaji wa elimu hii ya tarakilishi kwa hizi wadi ambazo zimepata fursa hii. Ijapokuwa katika wadi yangu hakuna vifaa kama hivyo lakini ni wazo zuri ambalo limeletwa na Kaunti yetu ili kuzindua na kufahamu mengi katika sehemu ya saa hii. Bw. Spika, saa hii elimu yetu ni ile ya vipaji; CBC (*Competency Based Curriculum*) na inategemea sana uzinduzi wa wanafunzi, lakini cha kushangaza ni kwamba ni kama imeenda ikaekelewa lakini hakuna ufwatilizaji maana hakuna *internet* ama marekebisho na kufuatilia hizo tarakilishi. Tulienda kuona utadhani hapo ni magofu; zimeekwa kwa meza, na nyengine ni chafu, vumbi na kwengine hata walimu hakuna. Wanafunzi ni wengi lakini watajifunza vipi katika hali hiyo?

Nia ilikuwa nzuri lakini tunaomba Kaunti ya Kilifi, dunia imegeuka lakini sisi bado tuko vile vile maana ukifanya jambo kama hilo ni nzuri lakini kama hutapalilia na kufuatilia basi hujafanya kitu. Maguu yamejaa katika Kamati ya *ICT* na tuone pesa zimewekwa na ziwe na uwezo wa kufuatilia ili wanafunzi wetu wapate mafunzo.

Bw. Spika, nafikiri tujaribu hata sisi pia tuone vile tutafanya maana...wacha nikomee hapo kwa wakati huu mambo mengine tutazungumza kwa wakati mwengine. Asante.

The Speaker (Hon.Mwambire): Hon. Zia.

Hon. Zia: Asante sana, Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii na pia nishukuru Mungu kwa neema zake ambazo ametupa mpaka tuko hapa. Kulingana na hii Ripoti, mimi nikiwa mmoja wa hii Kamati ya *ICT*, tuliweza kuzuru hivi vyuo na pia sehemu ambazo ziliwekwa *internet*.

Kuna mambo ya kufedhehesha sana. Kama alivyotangulia mheshimiwa Brown, ni kweli kila mahali ambapo tulikuwa tukitembelea kwanza kabisa hakuna vile vyumba ambavyo tulikuwa tunatarajia kama Kilifi kuweka hizi tarakilishi.

Pia, tukiangalia yale mazingira ambayo yalikuwa ni kwamba sehemu ambazo ni chafu ni sehemu zile *computer* ambazo zimeharibika watu wanazitupa tu. Ukiwauliza ujue katika *Department* hii tangu tulipoingia katikia uongozi hii *regime* mpya je, kuna maofisaa wowote ambao wameweza kutembea katika hizi *vocational centres* na kuona kama kuna changamoto ambazo mnazipata? Wakasema hakuna mtu yeyote ambaye ameweza kututembelea. Kwa hivyo tunarudi pale pale kwa kusema kwamba wale wahusika kidogo wamelegea na inastahili kuamka na kufanya kazi. Zile *computers* na vifaa vyote ni pesa za umma ambazo mwananchi anastahili kujua ilitenda kazi gani.

Tukiangalia kila mahali utapata *connection* ya *internet* ilifanywa lakini baadaye ikatolewa. Ukiangalia kama ni *lab* hakuna, *furniture* ambayo ni makabati na meza pia hakuna.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Tulikuwa tunasema hata tutakuchukua Spika pia na wewe ukaone pia yale mambo ya kufedhehesha.

Pitieni hiyo Ripoti na mtapata kwamba kuna mashaka mengi. Watu walisema kwamba iko lakini ukitembea hapo Buntwani ile *internet* ambayo iko inafedhehesha. Watu kumi na tano tena haiwezi kuwatoshesha. Ukienda hapo Mazingira *Park*, wanakuambia hapa ni wawili ama watatu ndio wanaweza kupata hiyo *connection* lakini ilitangazwa wazi kwamba ukifika mahali pale upata watu wengi na kuna hela ambazo tutazipata kwa sababu watu ambao walikodisha, watu watatoka mbali pengine hata bara kuja kujivinjari katika hizi sehemu zetu wakiona kwamba *internet* ya Kilifi iko shwari lakini wakifikia hakuna. Kile ambacho kinasemwa kiko tofauti na kile ambacho kiko kwa *ground*.

Kwa hivyo, ni lazima maofisa wetu waje na mipangilio mahususi kuhusiana na hili swala la *internet*. Hivyo hivyo tukiwa tunazungumzia swala la kule, na hata pia hapa kwetu Bunge pia nayo iweze kurekiebishwa, mheshimiwa Spika. Itakuwa ni aibu kwamba tuko hapa halafu unapata kwamba hakuna *back-up*. Ni swala ambalo lilizua utata sana. Kwa hivyo, mheshimiwa Spika tukiwa tunazungumzia yale ya kule na haya ya hapa kwetu pia nayo tuyaangalie na tuweze kurekebisha ili kila mmoja abebe msalaba wake. Kila mmoja ajukumike kwa ufasaha katika kazi yake. Kama ni mimi Zia ambaye nahusika ni lazima ni *show cause* ...

The Speaker (Hon. Mwambire): We have an intervention from hon. Munyoki...

Hon. Munyoki: Asante, mheshimiwa Spika. Mheshimiwa angetuelezea kwa uzaidi, sikumuelewa aliposema kwamba *internet* ya hapa haina *back-up*, labda atuelezee ki vipi?

(Laughter)

Hon. Zia: Mheshimiwa Spika, nilikuwa namanisha mitambo ya hapa, mara nyengine huwa inapotea kama juzi wakati Gavana alikuwa akihutubia. Tulipoangalia sehemu ile ya mafuta kulikuwa hakuna. Ndio nasema kuwe kuna *back-up*, kama tunakujua hapa hii mitambo iwe imechunguzwa na iko sawa. Asanteni sana.

The Speaker (Hon. Mwambire): Lakini hapa Bungeni pia mliona shida ni mafuta ama ni *internet*?

(Laughter)

Hon. Munyoki: Thank you, Mr. Speaker, for giving me this opportunity. I would like to commend and thank the ICT Committee; they have done a good job. From the Report, I have made a good observation that most of the VTC Centres seem to have a common problem. The computers were purchased in 2017 and we are in 2024; almost eight years. I think if some are not obsolete then most of them are not able to access more and current packages on offer. It is a waste of county public funds and I think maybe the Department needs to make a follow-up with the Director and the Chief Officer in charge to prepare a proper budget for the running and maintenance of these centres so that we may be able to provide, and people get service of the money that was used to purchase this equipment.

Finally, we would like to recommend to the Committee on ICT to have a look at the gadgets in the Assembly and may be come up with a Report on what is the problem. Thank you, Mr. Speaker.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Mkadi: Asante, mheshimiwa Spika. Nachukua huu mda kupongeza hii Kamati kwa ile kazi ambayo walifanya. Utaona kwamba katika kila sehemu ambazo Kamati ilitembea utapata kuna *computer* ambazo zilinunuliwa na katika hizo sehemu ni *computer* kidogo ambazo zinafanya kazi. Nakumbuka lile Bunge la Pili nilikuwa mwanakamati wa Kamati hii na mda ule pia tulipata nafasi ya kuzizungukia na shida tukapata bado ni hizi na tukaweka zile *recommendations* ambazo zilikuwa ni wale watendakazi wazishughulikie lakini inaonekana hakuna kitu ambacho kilifanyika. Ni bora labda kila sehemu ya hizo *vocational centres* iwe na *computers* kidogo lakini ziwe zinafanya kazi. Haitakuwa vizuri pesa za umma zitumike halafu *computer* zinunuliwe 20.

Katika zile ishirini (20) unapata labda tano ndio zinafanya kazi. Hakuna mipangilio ambayo wale maafisa wahusika watakuwa wanazungukia baada ya muda gani ili kuangalia hali ya zile *computers*. Itakuwa jambo la kufadhaisha maana hizi ni pesa zilitumika na kama mnenaji aliyetoka alivyosema kuwa ni zaidi ya miaka minane sasa. Kitu kilichowekwa mahali kwa miaka minane na hakifanyi kazi ni vizuri hiyo Kamati iendelee kufwatilia hili jambo na pia Wizara husika itilie mkazo ule uamuzi wa Ripoti hii ili linalohitaji kufanyika lifanyike kwa manufaa ya mwana Kilifi. Asante na naunga mkono.

Hon. Tete: Asante, Mheshimiwa Spika. Nataka kusema kwamba ni mwaka na zaidi toka tuingie katika mamlaka. Tulipoingia kwenye mamlaka, Kamati ziliundwa na wengi walio katika Wizara husika walipitia kwetu kuja kuwaidhinisha kwamba wana uwezo wa kufanya hii kazi tofauti na waliokuweco. Sasa tunaweza kupima na kujua uzani wa hawa wahusika kama wana uwezo wa kusukuma hii Kilifi mbele au la. Ishara yake ni kwamba ikiwa wanahitaji msukumo tutasukuma. Tabia haina tiba. Kuna wale waliotafuta kazi kwa sababu ya masilahi lakini utendaji kazi hauko kwao wana hesabu kalenda ni lini siku zitaisha mshahara uingie pasipo kuifanya ile kazi ambayo inafanya ule mshahara uingie.

Itakuwa ni aibu kwetu kama wana Kilifi maeneo ambayo tunayatengemea kwamba yatupe sifa na hadhi kama vile mazingira iwe tunapata habari *coverage* ya mtandao ina uwezo wa kumiliki watu wawili pekee sioni kama inapeana sifa kwa gatuzi letu. Nataka kukumbuka manifesto ya Mheshimiwa Gavana wakati akiwa nyajani alisema kutakuwa na mitandao wazi tena huru itakayokuwa inafanya kazi wakati wowote. Leo ni aibu sehemu kama hizi tunapozipitia tunapata kwamba hakuna chochote kilicho karibu na kile kilichosemwa.

Sina sababu za kumlaumu Gavana ila tuliowapa nafasi; hawayazingatii yale yaliyo katika *manifesto* wamelegea kuifanya kazi tuliyowapa, katika VCT, tuna imani kubwa ya kwamba wanafunzi wetu wanapopata nafasi ya kufundishwa elimu ya kisasa kupitia kwa vifaa hivi vya mitandao huwa tunawapa hatua kubwa ya ufahamu kwa elimu na maisha ya baadaye. Kama waliotangulia sakafuni wamesema ya kwamba dunia imebadilika. Hiyo ni kumaanisha kwamba teknolojia inapanda lakini watoto wetu wanabaki pale, katika lugha za zamani inasemekana kuwa wanabaki wakiwa *analogue*.

Wahusika wa hii *Department* ambao wengine walikuja hapa tukawa-*interview* na wakaonekana kwamba wanaweza saa hii wameashiria kwamba hawawezi. Naomba wapewe ufahamu ya kwamba Kilifi tunataka isonge mbele kwa kila hatua na wasiturudishe nyuma. Ikiwa ni kitu ambacho hawakiwezi sisi tumejua ni wapi wanatupeleka. Naomba kuchukuliwe hatua juu ya wale walioshikilia hii Wizara na pia watuletee Ripoti kuhusiana na yale tunayoyasikia. Asante kwa nafasi hii. Pia naomba yale ambayo Bunge hili yanayazungumzia yachukuliwe hatua yenye uzito.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Ray: Asante sana, Bw. Spika. Nachukua nafasi hii kupongeza Kamati kwa Ripoti hii ambayo iko mbele yetu leo nimeangalia ndani sana na nimenukuu vitu vingi vilivyoandikwa hapa vinaambatana na hali halisi ilivyo ndani ya wadi zetu kuhusu hizi VTC (*Vocational Training Colleges*) na kwenye mitandao. Hali kule haiko sawa na nashuku hali hii ilianza wakati wa *procurement*. Vile vyombo vinavyoletwa pale haviko katika ile hali hitajika. Hii inachangia hali ngumu ya kushawishi mwanafunzi kwenda kusoma pale. Kuna mashini tofauti tofauti kama cherehani na zingine utapata mwalimu hana ujuzi wa zile mashini wala hajui kuzifanyia *maintenance*.

Tunajenga shule kwa bei ya juu na vifaa kwa bei ya juu lakini kwa kukosa usimamizi mzuri shule zinakosa kusaidia wananchi na ni pesa za umma. Ripoti hii ni nzuri Kamati imefanya kazi na wahusika kwa Wizara itabidi tuwakazie kamba ili waweze kufanya kazi zao sawa sawa. Itakuwa makosa kijana aache kwenda katika hizo VTC kwa wadi yake na aende *college* nyingine kusomea kitu ambacho kiko katika hizo VTC tena kwa bei rahisi.

Hon. Ziro: Asante sana, Bw. Spika. Nimesimama kuunga mkono hii Ripoti na mapendekezo yake na hususan katika kuongeza mgao wa fedha katika hii wizara ya ICT. Ulimwengu umebadilika tunatoka *analogue* na kuelekea mfumo wa kutumia *internet*. Tutakapongeza bajeti kwa ICT tutawezesha vijana wetu kupata ajira. Hizi *computer* zilizo kule kwenye VTC nikipeana mfano wa VTC iliyo katika wadi yangu Hademu Polytechnic, kusema kweli hii shule haijajengwa; iliyo pale ni *container* na *course* ambayo ni moja inayofundishwa pale ni cherehani. Hii *computer lab* ambayo inasemekana iko pale mimi ningetaka kujua iko upande gani maana ninavyojua hakuna mwalimu anayefundisha hili somo la ICT. Kwa hivyo, ni changamoto kwa sisi kama Kamati na Idara ya ICT kuhakikisha ya kwamba mbali na kutekeleza mapendekezo ambayo yako hapa lakini pia tufanye uchunguzi zaidi tuone ya kwamba hivi vifaa ambavyo vilipelekwa kwenye VTCs zetu vitumike kwa njia inayofaa. Asante.

The Speaker (Hon.Mwambire): Hon. Twaher.

Hon. Twaher: Asante sana, Mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii. Kwanza nipongeze Kamati kwa kazi nzuri waliyofanya na nikinukuu kuhusu Muyeye VTC. Bw. Spika, Kamati ilitembelea chuo cha ufundi cha Muyeye na walishuhudia tarakilishi ishirini na tano (25) zilipeanwa katika shule hii lakini kwa bahati mbaya hakuna *internet*; utaniwia radhi kwa hiyo lugha. Upande wa *internet* haijawekwa pale shuleni kwa hivyo ni ngumu wanafunzi kupata mafunzo ya *computer*. Jambo lengine ni Buntwani *Waterfront*.

Pale katika bustani kuliwekwa *internet* lakini imewekwa kwa kiwango cha chini sana. Ni mapendekezo naweka katika Bunge hili uchunguzi ufanywe kwa mwenye aliyepewa kandarasi ya kuweka *internet* pale ilikuwa inafaa iwe ya kiwango gani na aliweka gani. Tunaona wanakandarasi wakilipwa pesa nyingi kuweka huduma ambayo ingesaidia watu wa Kilifi lakini wanaweka huduma za chini ili kujifaidisha kwa fedha zile. Ningependa kupongeza Kamati hii kwa kazi nzuri wameweza kufanya kutembelea vyuo vyetu. Kuna uwezekano sisi tunapitisha bajeti ili watu wetu wafaidike kule lakini ikifika katika utendakazi pesa zinafujwa. Asante.

The Speaker (Hon.Mwambire): Hon. Ngome Kalama.

Hon. Kalama: Thank you, Mr. Speaker, Sir, for giving me this noble chance. Being one of the Committee Members, I stand to support this Report. There is a need for thorough intervention in the programmes on the VTCs for it is paramount. This is an indication that value for money was not taken into consideration, so I stand to support this Report. Thank you.

(Question, that the Mover be now called upon to reply, put and agreed to)

Disclaimer: The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.

Hon. (Ms.) Faith: Thank you, Mr. Speaker. First, I want to thank the hon. Members of the House who have given their input to this Motion. I want also to thank the Committee for their hard work. The work we did moving around Kilifi County to see the status of the VTCs was very tedious work. I also want to acknowledge the common problems that have been stated by the hon. Members in the House. It is true that we are suffering the fate of obsolete machines, maintenance and machines are very dusty. There are no computer labs, and no internet connection, which is a common problem for all VTCs. Some of the VTCs do not have computers and we have heard from hon. Ngirani he borrowed from Jaribuni and Vitengeni. In the ICT hubs, the bandwidth is less, it cannot contain even a few people within. We also have a common problem with tutors. The computers were sent and there are no tutors to teach the students.

Hon. Speaker, that is the main reason why we came up with these recommendations and I will tell the House to refer to page 15 where the Committee put the recommendations so that they can be heard by all the Departments. We said having considered the information from the Committee's research it was recommended that there was a need to increase the bandwidth to all public hotspot areas to serve at least more than 100 users at a time. I think this will address the problem.

Another recommendation by the Committee is that there is a need for more allocation to equip the VTCs on ICT Hubs so that they can be able or act as information resource centres to benefit the communities in their catchment areas. Another recommendation is that we need to enact legislation that will enforce operations on VTCs and offer guidelines on their day-to-day activities. We made five recommendations and I beg to read them all so that you can know we worked hard; Development of united infrastructure to enable education digital content sharing in the VTCs, to promote E-learning in VTCs for digital skills. All the issues have been captured. The last one there is a need to have routine maintenance of all VTCs by the officers from the Department.

Mr. Speaker, I beg to thank the House for adopting this Motion because it is beneficial to all Kilifians. We are doing this for the benefit of all Kilifians and for that I say thank you very much.

The Speaker (Hon.Mwambire): Hon. (Ms.) Faith is very happy that Members have adopted the Motion, and we are yet to put the Question. Allow me to put the Question so that we can confirm whether she will be happier.

(Question put and agreed to)

MOTION

GOVERNOR'S SECOND ADDRESS-THIRD ASSEMBLY 2024

Hon. Tete: Thank you, Mr. Speaker. On behalf of the Leader of Majority, I take this opportunity to move the Motion: -

THAT, the Thanks of the County Assembly be recorded for the exposition of Public Policy contained in the Second Address of the Governor His Excellency Gideon Maitha Mung'aro, OGW delivered on Wednesday, 13th March 2024.

Thank you. I call upon hon. Twaher to second.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

(Hon. Twaher seconded)

(Question proposed)

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Members, kindly make your requests.

Hon. Shehe: Thank you, Mr. Speaker, Sir. I stand to appreciate the Report before this House by His Excellency the Governor. We realize that we have had several attempts at questions that were not answered very vividly because we have not been accorded most of the information but this Report is very conclusive and I wish to appreciate that in any respect after all what we were expecting, there are one or two issues that I have seen that have to be approached very fast indeed like the recruitment of the County Public Service Board, there are two Members that are still missing and I hope His Excellency is aware and he commented on the same that he is going to make sure that those two slots are going to be filled as early as possible. Now, our observation is such that as the County Public Service Board is being constituted, I would like to comment that it expedites the recruitment of the very many youths that are waiting outside.

I hope this one is a very valid contribution from His Excellency and I stand to appreciate and ask our Members to see it positively that most of the points that were aligned here touched his manifesto as per his campaign time. Thank you, Mr. Speaker, Sir.

Hon. Kea: Thank you, Mr. Speaker, Sir, for giving me this opportunity and I would like to first thank the House for making it possible for us to go through this speech which was delivered to us by His Excellency, the Governor.

Again, I want to express my dissatisfaction with what happened on the very material day when the Governor was giving his speech and the power had problems. Some of us had to rest our eyes because we got bored somewhere. Again, I would like to commend the good job that the Governor did, especially pinpointing some areas that I am part and parcel of.

Let us talk about the education sector; he assented to the Scholarship Act where we were dealing with Kshs350 million up to one billion shillings on the maximum and minimum of Kshs500 million to make sure our children go to school. This was a good thing that he did and indeed he captured it in his speech. As we are seated here, there are some students who are still at home due to laxity by their parents, but on our part as a county we have done our level best to make sure that we have given enough money for them to go to school. So, I thank the Governor for putting it to the public so that they could understand what is going on.

Again, on page 20 he talked about the Wezesha Fund. Many of us in the Trade Committee have been trying to see how much money has been given out through the Department of Trade, Tourism and Cooperative Development but he did put it very clear here so that we could see, read and understand and this is a wonderful job that the Governor is doing. I understand his speech was going in tandem with what he had promised people during his campaign trails when he was looking for the Governorship of this county. I congratulate him for capturing so many things which answered a lot of the questions that we were asking ourselves. Good job, Mr. Governor and God bless you. Thank you. I rest my case.

Hon. Munyoki: Thank you, Mr. Speaker. I would like to congratulate the Governor on two key areas. The first one is on the school feeding programme whereby 812 have been provided with porridge and this has increased the number of our children going to school

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

because mostly the drought conditions many of our children were not attending school. I would like to commend the Governor on this aspect and urge him to continue so.

Secondly, on the issue of title deeds, over 800 title deeds were issued and being a member of the Lands Committee we would wish to support him and urge him to push more so that most of our members who own land but have no documents, this will be a very big step forward in assisting our people to get the proper documents which we will be able to support them in case they need financing from local institutions. With those few remarks, I beg to commend the Governor. Thank you.

Hon. Brown: Acha nishukuru tena kwa nafasi hii. Napongeza hotuba ya Gavana. Ilikuwa ni hotuba ambayo ilikuwa na uzito mwingi. Ilikuwa na mambo mengi ambayo yamefanyika katika kipindi kidogo ambacho ameshika hatamu. Kulingana na *manifesto* yake na pia *manifesto* hiyo iliandamana na vile pia sisi tulikuwa tukifanya kampeni hasa wakati ule tunazungumzia swala la elimu jinsi watoto watachukuliwa na kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi atapata fursa ya masomo. Hata kama hatujafikia kile kiwango cha kuwezesha kila mtu lakini angalau kuna uwezo fulani ambao tumefanya. Pongezi kubwa ni kwa hili Bunge; sisi waheshimiwa tumeshikana, watu walisema ukiona vyaelea jua vimeundwa.

Wanafunzi walipata nafasi ya kwenda katika shule za kitaifa. Hiyo ni bidii ya Bunge hili kujizatiti pamoja na maono ya Gavana wetu ili kuunda Msawaada ama vipengele ambavyo vitahusisha hii kazi ifanyike. Tunashukuru kwa sababu Gavana sasa amefaulisha jambo hili watoto wengi wameenda shule na sifa ziko kwa sababu ya kazi hii. La kushukuru zaidi ni kwamba hakukuwa na ubaguzi kwamba kuna shule za kibinafsi wale wanafunzi wa serikali walichukuliwa wote kuwa wanafunzi waliofaulu. Nalipa kongele Bunge hili na pongezi kwa Gavana kwa kazi njema. Upande wa chekechea madarasa yako mengi na mengine yananiwa kujengwa.

Jambo lingine ni kuhusu swala la *municipality*. Mtu ukitaka kukuwa lazima ujipanue na ukitaka mji wako uitwe mzuri lazima ujenge. Sasa tunashukuru kwa kuwa Kilifi tumeijenga kwa sababu kupanua mji wetu kwa ajili ya ukuzaji wa uchumi. Tukizungumzia kuhusu *municipality* ya Mtwapa ambayo imeenda hadi katika Wadi ya Junju na pia katika Wadi ya Mtepeni. Ombi langu katika mambo ya *tourism, trade and cooperatives* ni kwamba Gavana alisema ataweka barabara nzuri za lami. Kule kwangu ni msitu. Kuna jamaa wengi wa vipanga wanajificha sana kule sehemu za mahotelini. Mji mkubwa wa Mtwapa unaokua katika masaa 24 kila siku ukifanya biashara hawana hoteli ambazo ni za kitalii, bali hoteli zote za kitalii ziko katika Wadi yangu ya Mtepeni. Kuna hoteli kama *Salama Beach*, kuna *Jumuiya Resort*, kuna *North Coast Beach Hotel*, kuna *Sun N Sand* halafu kuna Sultan ambayo inamilikiwa sana na wachina. Kule ni msitu hakuna mipangilio ambayo imeanza kufikiriwa ili kupelekwa katika hizi sehemu. Kuna Hotel za Sultan na *Sun N Sand* wao wenyewe walijijengea barabara. Jinsi tulivyopata hii *municipality* wawekeze zaidi ili mji wetu wa Mtwapa ukang'are kwa upande wa sekta ya mahoteli na tupate kodi zaidi.

Mambo mengi yaliyoangaziwa hapa ni ya ukweli na ya kufurahisha sana. Napongeza na kukomea hapo.

Hon. Thaura: Asante sana, Mheshimiwa Spika, kwa nafasi hii. Nataka kuzungumzia hotuba ya mheshimiwa Gavana. Sikupata nafasi ya kufika kwa sababu nilikuwa na afya yenye mgogoro, lakini nilifwatilia Hotuba moja kwa moja kupitia mtandao. Poleni kwa changamoto zilizowapata siku hiyo. Hili ni Bunge ambalo linaweza kuthibiti maswala hayo yasiweze kutokea tena. Nataka kumshukuru Gavana kwa kile ambacho alikifanya kujaribu kugusia kila sekta kwa

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

upana kulingana na alivyoweza pamoja na mawaziri wake. Tunapojadili hutuba ya Gavana isiwe ni kutaja tu sifa; huo ni unafiki mkubwa sana, kwamba tunashukuru hotuba ni nzuri sijui kama tunamsaidia kwa kusema ilikuwa nzuri tu. Zipo sehemu zilizo na mianya ambayo sisi kama wawakilishi wa wananchi, tuna nafasi ya kuzidi kumuelekeza Gavana na timu yake na hilo ndio jukumu letu kama Bunge. Kwa hali hiyo hatuisaidii serikali; sisi wenyewe tunapokosa kufanya kazi yetu ya *Oversight* vizuri basi moja kwa moja tutakuwa sababu kwa nini serikali imekosa kufanya jukumu lake.

Bw. Spika, yapo mazuri mengi yaliyozungumzwa na Gavana lakini tukubaliane hakuna mtu wala taasisi y iko asilimia mia. Ilitajwa miradi ya upande wa afya, elimu, talanta, mambo ya biashara upande wa *Wezesha Fund*, maji na pia miradi ya *flagship*. Wacha niongee kuhusu hii *Wezesha Fund*; Bw. Spika, utakubaliana na mimi kwamba kumekuwa na shida kubwa sana upande wa hiyo *Fund*. Kwa ile wadi ninayowakilisha ni moja katika zile wadi ambazo hazijafaidika kikamilifu kwa sababu zile *bank* zilizohusika katika kugawanya *form* na kuhakikisha kuwa wananchi wanapata pesa hawaji mashinani; nahisi kuwa wamezingatia sana sehemu za mijini, wako na jukumu kama watendaji kuhakikisha kwamba wameshuka zaidi mashinani kuwapa wananchi hamasa na kuhakikisha kwamba wananchi wanajua ni zipi faida za kujiunga kama makundi ama kusimama kama wanabiashara binafsi na kupata pesa hizi.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mmoja wa wana Kamati wa Bajeti na nitaliweka wazi. Ile bajeti iliyopita nilitofautiana sana na wenzangu ambao tuko pamoja kwa hiyo Kamati. Sababu kubwa ni kwamba nahisi kwamba ziko Wadi ambazo waheshimiwa wako na ushawishi moja kwa moja na Serikali na huu si mjadala ambao ni wa kuficha. Wako waheshimiwa ambao wana ushawishi wa moja kwa moja na serikali. Wamelichukulia hilo kama faida kwao kwamba wana uwezo wa kusukuma miradi yao ukitofautisha, Mheshimiwa Spika, na wengine ambao ushawishi wao kidogo umepungua kwa sababu moja ama nyingine za kawaida za kibinadamu.

Ukizingatia namna pesa zinavyopelekwa katika Wadi hata saa hii tukifungua hiyo bajeti yenye imebidi tuangalie kila wadi *vis-a-vis* wadi nyingine, unaweza pata kuna wadi nyengine wamepata ile tunaita the *lion's share* na kuna wengine ambao wameenda nyumbani na kitu kidogo sana ikiwa mimi ni mmoja wao.

Nataka niunge mkono kile ambacho Mheshimiwa Karisa Ngirani...

The Speaker (Hon.Mwambire): Wewe ni mmoja wa kupata pande kubwa ama pande dogo? Unajua hujafafanua vizuri mheshimiwa.

Hon. Thaura: Wale waathirika.

(Laughter)

Nataka niunge mkono na nimpongeze Mheshimiwa Ngirani kwa ule Mswaada ambao haujafika Bungeni lakini bado anautayarisha. Wacha nikwambie tunaubiri kwa hamu na ghamu na tunaendelea kuambizana kama waheshimiwa kwamba hatuhitaji mapenzi ya mtu yoyote kuhakikisha ya kwamba tunataka pesa. Iwe kuna sheria ambayo italazimisha kila mheshimiwa kupata pesa. Awe ana ushawishi awe hana ushawishi lakini wapate pesa kwa sababu ni pesa za Kilifi lakini sio sababu ya mapenzi. Hayo mapenzi yaendeleo mimi sikatai lakini iwe sheria inamteteta mwana Kilifi popote atakapokuwa.

Nimetangulia kusema sisi tukiwa katika jukumu letu la *oversight* tunaisaidia serikali. Ikiwa kila mahali Kilifi hii mheshimiwa Gavana amefanya mradi kwa sababu kumekuwa na usawa, basi itakuwa haogopi kwenda mahali popote. Anaweza kuja Sokoke, Magarini akaongea

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

na wananchi wake kwa sababu kila mahali amegusa. Kwa hivyo, ni makosa kutengwa lakini lazima turekebishe na kurekebisha ni sisi tusimame na msimamo kama huu tunaoupanga. Kwa hivyo, tunampongeza Mheshimiwa Gavana lakini tutamsaidia mahali ameteleza tutasimama naye ndio mwisho wa siku akifanya vizuri, sisi wote tutakuwa tumefanya vizuri. Asante sana.

Hon.Tete: Asante tena, Mheshimiwa Spika, kwa kunipatia hii nafasi. Ningependa kuzungumza machache. Mgala muuwe na haki yake uumpe. Naona kuna haki ya mimi kusifu Hotuba ya Gavana nikienda moja kwa moja kwa Kitengo cha Afya. Mheshimiwa Spika, ni kwa miaka mingi huduma za *ambulance* zilikuwa zinalipishwa kwa wananchi wetu wa Kilifi. Mara mheshimiwa alipoingia uongozini garama hizi za *ambulance* zilitolewa na zikapeana afueni kwa mwananchi anapopatikana na dharura. Kwa hilo sitasita kusema kongole Mstahiki kwa sababu umewaona wananchi wako pale ambapo walikuwa wanataabika.

Pili, ninaenda katika Kitengo cha Elimu. Kilifi yetu watoto wetu bidii walikuwa nazo na wazazi walikuwa wanajitahidi pale walikuwa wanaweza kuona ya kwamba watoto wao wanapata elimu bora. Lakini kuna mahali walikuwa wanalemewa mpaka watoto kufikia mahali pa kuwachia masomo katikati. Ukiangalia wale walikuwa wanaathirika ni wale watoto werevu ambao sisi kama wana Kilifi tungewategemea kwa nyadhifa za juu kwa miaka ijayo. Kuletewa mradi wa *Scholarship* Kilifi ni hatua kubwa sana na nyanjani watu wanaifurahikia hatua hiyo na sisi ni mashahidi wa mambo haya. Sitasita kusema kongole kwa Gavana kwa yale anayowafanyia wana Kilifi.

Tatu; nataka niunge mkono aliyetoka sakafuni kwa kusema ya kwamba kwa kumpa sifa Gavana huwa hatumsaidii. Lakini vile vile nataka kusema pale ambapo amefanya inafaa kuambiwa amefanya lakini pale ambapo hajafanya si kwa sababu hataki kufanya labda hujamsongelea na kumpea ushauri ili haya malengo yatimiye. Kwa hivyo, tunampa sifa pale anastahili kupewa sifa kwa kufanya ikiwa tumeona na pale ambapo hajastahili kupewa sifa hatutampea sifa, si kwa sababu amefanya vibaya labda hajafanya tunavyotarajia. Labda angefanya lakini kwa sababu hiyo basi ningesema tuwe wepesi wa kumsongelea bila kumuogopa. Yeye ni mwanadamu. Wale tunasema wako karibu na serikali ladba walitafuta namna ya kumsongelea na wakapata faida za kuwa karibu naye.

Sisi tunakubaliana na Msawaada utakaoletwa na Mheshimiwa Ngirani kwamba ikifika waheshimiwa wapate haki sawa. Hilo nitakubaliana nalo lakini vile vile haki utakayoipata kuna mwengine atasongelea na ataongezwa zaidi. Urafiki ni sawa na mtegemea nundu hataacha kunona. Kwa hivyo, ukijisongelea hata ile haki ukipewa ukimsongelea bado utapata zaidi. Mheshimiwa Spika, ninarudi nikisema ya kwamba ni mengi ambayo yamezungumzwa katika Hotuba na Gavana nampa kongole tena kwa kupokea maombi ya maeneo matatu. Moja wapo ikiwa Mariakani, Mtwapa na Watamu miji ambayo ameipandisha hadhi kufikia kuitwa Manispaa kwa kuungwa mkono na Bunge hii. Hizo ni hatua za maana sana na zitaboresha maisha ya wana jamii katika maeneo hayo. Itatoa ajira kwa wana Kilifi na hayo ndio maendeleo ambao tulikuwa tunataka. Nina hakika kwa miaka hii mitano mengi ambayo yalikuwa yamewachwa nyuma yatafanyika.

Ni ombi langu hii Hotuba imfikie Mstahiki ya kwamba japo ana nia ya kuiinua Kilifi na kuifikisha mahali alipotamani, katikati ya Serikali hii kunao wana tamani kumrudisha nyuma na hapo ndio nasema azidi kuwa makini kwa sababu hata yale ambayo tunayaona hapa ndani ya Bunge kama wengine walivyotangulia hapa sakafuni ni kwamba kuna utepetevu wa utendakazi katika hii Serikali. Mfano, hata hapa kwetu tu ndio tupate dhiki na aibu kama zile tunazozipata kwa mfano mheshimiwa Gavana alipokua. Ni kwamba kuna mtu alikua amelegea mahali ndio

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

tukafikia mahali pa kukumbana na ile aibu. Imekuwa ni aibu kwa sababu ukiingia mitandaoni utaipata inazungumziwa na sababu ni mtu kujisahau. Chenye anaangalia yeye ni mshahara lakini kazi iliyomleta haizingatii na mheshimiwa Spika, jumba ni kubwa hili lakini lina mengi ambayo saa hii tukiyaingilia tunaona kwamba ni wengine labda hawafiki kazini.

Utanisamehe, mheshimiwa Spika. Saa hii nilikuwa nimeenda kujisaidia sehemu nyengine nimezipata hazifanyi kazi, na kuna mtu mhusika. Ni hali ambayo ni kana kwamba hii serikali yetu watu wanatafuta mwanya wa kuja kuchukua pesa ya umma kwenda kujifanyia mambo yao lakini si kufanya kazi. Watu wa aina hiyo ningeomba wachukuliwe hatua. Wasituaibishe. Tuliingia katika hii serikali kwa malengo ya kutaka kugeuza serikali kutoka uovu hadi uzuri kwa hivyo, mheshimiwa Spika, nasema asante kwa hii nafasi na naomba hata hapa pia tusizungumzie ya nje kwamba *Executive* kuna mahali kunaenda kombo, hapa kwetu pia kuna shida na tungeomba vile vile tunavyokua wakali kwa upande ule hata hapa pia hatua zichukuliwe za kisawasawa.

Mengi ambayo tunaendelea kuyaangalia na ikifikia hatua ya kuchukua hatua tungeomba zichukuliwe ili kesho tupo ama hatupo wengine wajifundishe kufanya kazi wakijua kwamba ule mshahara ni pesa ya umma. Asante.

The Speaker (Hon. Mwambire): Waheshimiwa siku itakuja tutaongea ya hapa na ya humu, tuongee kuhusu hotuba ya Gavana. Msiwe na haraka. Mheshimiwa (Ms.) Mkumbi (Mariam).

Hon. (Ms.) Mariam: Asante sana, Bw. Spika, kwa fursa hii. Nimeiangalia hii hotuba na naweza kusema ni hotuba ambayo ilikuwa inapeana matumaini. Tukiangalia Gavana kuna mambo ambayo amejizatiti pamoja na serikali yake. Moja ambalo nampa pongezi ni swala la afya kwa sababu hiki ni kitengo ambacho hata ukisoma hii hotuba yake katika kitengo cha afya unapata kimeelezwa kiundani zaidi na katika hicho kitengo kuna mambo ambayo yamefanyika na kuna vitu vya kuonekana na kuna zile ishara ambazo ukifika pale utazona.

Kwa hivyo, nataka kumpa kongole kwa swala la afya lakini pale pale kwa afya, tunajua sisi sote kumekuwa na malalamishi mengi sana kuhusiana na ukosefu wa dawa katika zahanati zetu. Kwa hivyo, hii inamaanisha bado kuna kazi ya kufanya katika kitengo kile. Vifaa viko, ndio, lakini kama hakutakuwa na dawa tutakuwa hatujasaidia wananchi kwa sababu kama mtu amepimwa vipimo lakini baadaye aregeshwe kuwa dawa mpaka akanunue, yule mtu wa pale chini na kulingana na hali ya maisha utakuwa hujamsaidia sana.

Kitu chengine hapo kwa afya, nasema hiyo hotuba imeleta matumaini kwa sababu sisi wenyewe kuanzia tuingie na wananchi wetu kumekuwa na maswala mengi ya ajira; watu wanaulizia kuhusu ajira. Katika hiyo hotuba Gavana ametuonyesha kuwa yuko na mpango wa kuajiri ndio maana nikasema imeleta matumaini.

Kitu chengine ambacho na ambacho mheshimiwa wa Sokoke amekizungumzia ni kuhusu maswala ya ugavi wa hizi raslimali kwenda kwa zile wadi zetu. Kuna wadi ukisoma katika hiyo hotuba zimetajwa zikiregelewa katika kila kitengo na kuna wadi nyengine zinajitokeza mara moja, Hii ni ishara ya kuwa katika ugavi wa hizi raslimali za kaunti kuna wadi nyengine zinafaidi zaidi na ukiangalia matatizo yanafanana karibu katika kila wadi. Hapo ni lazima pia tuzungumzie ili kwamba wakati watu wanagawanya raslimali waweze kuangalia swala hili ili wananchi wote wa Kilifi wawe watafaidikia kwa pamoja. Asante, Bw. Spika.

Hon. Said: Thank you, Mr. Speaker. I want to congratulate the Governor for addressing this House and outlining his vision and agenda for the people of Kilifi County. I have gone through the whole speech, and I can say we should all support the programmes that ...

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Speaker (Hon. Mwambire): There is an intervention from hon. Thaura.

Hon. Thaura: Mheshimiwa Spika, ndugu yangu Said ana kizungu kizito sana leo ila nina wasiwasi anaweza kuwa anasoma mahali. Sina shida naye kwamba ana ufahamu huo wa lugha ya Kiingereza lakini kidogo naona macho yake yanatazama chini...

(Laughter)

The Speaker (Hon. Mwambire): Elewa yuko kwa mfungo, usiwe na wasiwasi.

Hon. Said: Mheshimiwa Thaura usitatizike na mimi.

The Speaker (Hon. Mwambire): Just proceed in English, hon. Said Juma.

Hon. Said: Usitatizike kabisa. Mimi hata huwa mara nyengine nashangaa unasema mheshimiwa Said ulaya kule, usitatizike. Ni mambo madogo tu haya. Kama vile unasema wewe ni *dozer* na juzi pia *dozer* lako lilikuwa halina cheni kwa hivyo kuwa mpole. Tuliza, ama vipi?

(Laughter)

Asante, Mr. Speaker... That he let in his address because they are very beneficial to our people. Mr. Speaker, Sir, I will highlight two issues in the address that touched me greatly. One is the establishment of an emergency medical service centre that is equipped with state-of-the-art ambulances and medical doctors at the Kilifi County Referral Hospital. This establishment and the massive investment in healthcare will ensure our county has access to quality health services.

Two is about water purification with the extension of water infrastructure and the sinking of boreholes across the county. Thank you, Mr. Speaker, Sir.

Mr. Speaker, nataka kushukuru sana ...

The Speaker (Hon. Mwambire): Hon. Said Juma, you either speak in Swahili or English. I gave you a leeway when you were responding to Thaura but since you have started in English, please proceed in English.

Hon. Said: Thank you, Mr. Speaker, I end my speech there.

Hon. Mkadi: Asante sana, Bw. Spika, kwa nafsi hii. Nasimama kuunga mkono hotuba ya Gavana. Tukianza na swala la Elimu ni hatua nzuri kwamba alilenga kusaidia wale ambao hawangeweza kuenda zile shule ambazo wameitwa kwa hatua ya kukosa pesa lakini ukiangalia vizuri kwa sisi ambao tuko mashinani utapata wegi waliofaidika na hizi pesa ni wale walio na uwezo na kidogo wale waliokuwa wamelengwa kufaidika na hizo pesa. Ni ombi langu kuwa wakati mwingine kitu kama hiki kikifanyika kuwe na nafasi nzuri ya kuchagua wale ambao hawajiwezi kweli kweli. Wengine *cheque* ziliandikwa na zikafika shule lakini kwa sababu yule mtoto kwao hakuna uwezo wa kumnunulia vitu vya kuenda shule ya kitaifa, hakuenda. Kwa wakati mwingine tulitilie maanani hilo.

Upande wa Wezesha, tukiangalia kule nyuma japo hapa tumepewa ripoti kuwa kuna makundi yaliyofaidika vile pesa zilivyotolewa, lakini kwa wale ambao hawana ufahamu hawakupata pesa hizi japo mtu angepata hata kama ni kiwango kidogo kingewasaidia kujinasua katika zile biashara ndogo ndogo kule nyanjani.

Upanda wa afya, mbali na kuboresha kuna umuhimu angalau kila wadi kuwe na zahanati ambazo zitakuwa na vifaa. Yale yanayofanyika katika hospitali kubwa basi yawe kiasi yanafanyika kwa hizo zahanati ili kupunguza msongamano katika hospitali kubwa. Sio vizuri kila mtu kutoka katika wadi yake kukimbia pale *complex*, Malindi ama Mtwapa.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Tukienda upande wa *Municipalities* twashukuru kwa kupata zile tatu; hii itoa nafasi za ajira. Maombi yetu ni kwamba wale watakaokuwa wanahusika na zile *Municipalities* wapewe nafasi nzuri ya kudhibiti yale mapato yatakayokuwa yakipatikana ili pesa zile wazitumie katika kupanua zile *Municipalities*.

Hon. Hinzano: Asante, Bw. Spika, kwa nafasi hii. Nataka kutoa pole zangu kwa kukatizwa kwa hotuba ya Gavana. Ni kweli kuwa wengi wana macho lakini huwa hawaoni. Mimi niliona jinsi ulivyokuwa ukijaribu kusoma hiyo nakala hadi *Serjent-at-Arms* akakusaidia na *torch* kabla ya hotuba ya Gavana. Kwa sababu nguvu za umeme zilikatika, ukakatisha kikao wakati ule kwa dakika tano na baadaye Gavana akarudi na hotuba ya Gavana haikukatishwa wala haikuwekwa vikawazo vyovyote. Lakini hii tabia ya ukiritimba wa siasa na kujenga mazingira mengine tofauti sio haki, waheshimiwa. Kwa sababu kilichofanyika ni kwamba Spika alipata shida sana kusoma nakala kwa kumuita Gavana lakini kwamba hajamuita Gavana akakatisha kikao na tukatoka, baada ya umeme kurudi Gavana akaja na akasoma bila kukatishwa. Huu ndio mtazamo wangu.

Nikienda kwa hotuba ya Gavana ni nzuri kwa wananchi wote wa Kilifi, japo kuna mambo fulani haswa ya mashamba. Ukiangalia ardhi zetu, kwa mfano kama mimi niko na *Sub-Location* tano ambazo ni Mongotini, Kakuyuni, Malimo, Paziani na Madunguni lakini kata ndogo ya Malimo yote iko ndani ya 10 *miles strip* yaani bado kuna mmiliki bwenyenye anayeambiwa hayuko lakini anamiliki na wananchi wangu wa Malimo ni *ma-squatter*.

Nashangaa sana kuona uhuru ulipatikana katika jamhuri yetu ya Kenya lakini kule bara kulikuwa na mashamba ya wazungu yanaitwa *white lands* lakini sasa zinamilikiwa na waafrika na watu wako huru. Huku Pwani bado kuna mabwenyenye ndani ya *mile* 10 eti ni mashamba ya watu ambao hawako hapa. Hili ni jambo la kushangaza na kushtua sana. Kama ni mwananchi wa Kakuyuni na yuko Malimo na anaishi kama *squatter*, ni maendeleo gani atafanya akiwa pale Malimo ikiwa yeye ni *squatter*? Lazima tutoe suluhu ya ardhi katika nchi hii yetu.

Huyo Waziri wa Ardhi azingatie haya sana kuhakikisha wananchi wa Kakuyuni hasa Malimo Sub-Location wanakuwa huru na kufanya maendeleo kwa sababu mipangilio ya Gavana ni mizuri.

Gavana ana mwelekeo mzuri. Shida kuna mambo aliyoyataja katika wadi yangu ambayo yanaendelea vizuri; uanzilishi wa barabara kutoka Goshi kwenda Madunguni-Kavinyalalo ambayo sasa iko katika awamu ya pili. Lakini pia alitaja ECD (*Early Childhood Development*) ya Kaliapapo ambayo shida ni kwamba walimandikia Gavana kwamba hiyo shule ya madarasa mawili iko tayari lakini mpaka sasa *contractor* hajapewa barua shida ni wale *procurement officers* katika maafisi na *Chief Officer*. Kuhusu hii hotuba ya Gavana, kuna watu ambao wako katika maafisi wanaomfanya Gavana kuonekana anayoongea sio kwa sababu hakuna madarasa yaliyojengwa Kaliapapo kufikia sasa. Wengine wamepewa stakabadhi za kuanza kazi lakini yule wa Kaliapapo bado na watoto wanatoka kilomita kutoka Kaliapopo hadi Arabuko Sokoke ndio wanaenda wengine wanaenda hadi Mongotini kilomita zaidi ya tatu tena na ni watoto wadogo. Kwa hivyo, hii hotuba ni nzuri lakini ndio huwa mara nyingi namwambia Gavana kwamba watu wanamfunga mkono awaleta hapa Bungeni ili tuweze kumsaidia kuwapeleka nyumbani ili tutafute wengine kwa sababu kazi zake na mipangilio yake ni mizuri lakini kuna watu wamefunga mkono katika maafisi.

Procurement Officers kusema kweli wanadhhalilisha sana *contractors* na *suppliers*. Wako na maneno mengi ambayo hawawezi kufanya miradi ifanyike kwa wakati. Ukiangalia kuna miradi mingi kwa kila wadi haijafanyika na sio kwamba hatukufanya kazi yetu ya kupitisha

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

bajeti hapa na tukamaliza na pesa ziko. Ni shida gani *Procurement Officers* wanahangaisha watu ati *network* hakuna, *system* iko chini kila wakati wanaambia *contractors* na *suppliers* maneno hayo. Miradi haifanyiki kwa uharaka katika wadi zetu.

Kwa hivyo, mimi nampongeza Gavana kwa Hotuba hii na mipangilio pia aliyoiweka katika Wadi yangu ya Kakuyuni na wana Kilifi hususan mambo ya ukulima na elimu, mambo ya barabara na mambo ya afya. Upande wa Afya kuna shida, Mheshimiwa Spika, kuna wale wasaidizi wa wale wahudumu wa afya kule nyanjani. Kuna mashirika ambayo yalikuwa yanawalipa lakini sasa yale mashirika wale wasaidizi wa wahudumu wa afya wamekuwa na kazi ngumu mapaka sasa wanashindwa na chakula. Hawajalipwa zaidi ya miezi tisa ama mwaka kufikia saa hii ni Ripoti niliyopata kwa wadi yangu. Ukiangalia wanafanya kazi ngumu sana ya kusaidiana na yule mhudumu wa afya pale kwa zahanati. Ni watu wa thamani sana na kwa nini wasifanyiwe mpango wakaingizwa katika malipo? Kama wanasaidia na wamekuwa zaidi ya miaka sita na wako hapo wanateseka. Kila siku wanasubiri mtu adungwe sindano ipatikane shilingi hamsini ndio walipwe. Wanaishi maisha magumu na wanahudumia watu ambao wengine wako na maradhi ambayo yanaweza kuwaambukiza afya yao.

Mheshimiwa Spika, kupitia kwa Gavana wetu naamini kabisa pamoja na hii Kamati ya Afya hapa Bungeni kuweza kushughulikia hili jambo maana hawa wahudumu wa afya wanapata kazi ngumu na wanasaidia wanachi pale. Hawajapewa kipau mbele. Ni ombi langu kupitia kwa Gavana hili swala liweze kuzingatiwa ili wahakikishe kwamba wanapata haki yao.

Nataka nikomee hapo na nishukuru Bunge hili na Gavana kwa muongozo wake. Tukiendelea hivi tutasaidia Kilifi kwa kuwa wazi tusijifanye kwamba sisi kazi yetu ni kusema ndio tu kila saa. Ni kweli unaweza kusema ndio lakini ndio yako, ndio ya wananchi pale mashinani? Ama ni ndio yako kwa sababu unapokea mshahara? Tuongee ule ukweli kwa sababu wananchi wanapitia hali ngumu. Haina haja ya kujipendekeza. Mimi kama nina makosa kama kiongozi wa hiyo wadi wana haki ya kuniambia. Hatukuja hapa Bungeni kuweza kutetea Rais, Gavana ama Seneta ama Mbunge. Tumekuja hapa kutetea wananchi, hilo lazima tulifahamu. Kama tutafahamu hilo tutaenda sawa. Kukosolewa si shida wala si matusi. Ukikosolewa unapatiwa muongozo ili mwananchi pale chini ambaye hawezi kuongea aweze kupata unafuu wa maisha yake. Asanteni sana ns nashukuru sana, Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon.Mwambire): Hon. (Ms.) Sidi.

Hon. (Ms.) Sidi: Thank you, Mr. Speaker. First, I want to thank the Governor for his speech and all that he said regarding the state of the County. As much as we want to thank the Governor, I want also to echo what my fellow MCAs have been saying about the real state of the county. Let us look at the Health Department, I think we have Reports that usually come. We have four equipped ambulances, so I do not know who misled the Governor and told him that we have five ambulances. I think we have four ambulances that we purchased. On the same note, on health, it is very sad that Mariakani Hospital does not have a doctor on a day-to-day basis. The Governor's first agenda is to ensure good health for the people of Kilifi. Every time the people of Kayafungo go to Mariakani Hospital, there is no doctor and no medicine. So, it is unfortunate that someone will tell the Governor they are doing their best and the real state of health is bad.

When you go to Ndatani Dispensary, it does not have doctors and nurses. The one that was there, the Department decided to move him from that dispensary and placed him in another dispensary. Tsangatsini Dispensary, we have the same problem, no doctors and medicine. When we go to Gotani Health Care, we have no doctors, no ambulance, no water and there is a maternity wing there. So maybe because you will agree with me, we want to see His Excellency,

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

the President. He said it is about time the MCAs call the CECMs to come to the Assembly to tell us what they are doing. Not this Committee business because committees are being answered but it is true that around our hospitals, we do not get proper medication, doctors and everyone that is usually there is a casual and this person has not been paid for the last six months. Those are the people that are attending to our people on the ground. It is about time for the CECM (County Executive Committee Member) for Health to come to this honourable House and maybe get a clear picture of what is happening because the stories of no doctors are everywhere and every time.

When we go to the Education Department, I think we have finished here with the ICT Department. There are no computers and no internet but here we have been reported that we have seven Vocational Training Centres with modern tools and equipment during the review. Kindly...and they have mentioned them here and these are the same ones we have been deliberating and saying they are not equipped. They are misleading the Governor by reporting that these Vocational Training Centers have modern equipment.

The problem at the ECD Centres is equally the same. We have ECD Centres right now where we have the young ones who are seated on the ground learning. The people who are being paid by the County probably are one teacher and now the common *mwananchi* must cater for two or three other teachers to pay for the learning of the children. ECD also is a big challenge to the community and when we sit here ECDE and Vocational Training are our major roles in terms of education in our community. If we go for our oversight roles, we might be able to help the Governor achieve his manifesto.

Third, on the Roads, Transport and Public Works Sector; I just want to say this sector has little to be desired. They have said so many things, but we are the ones who are using these roads. Every weekend we leave here and go to the ground. We see the state of the roads that we have. It is very unfortunate that a Member in your area cannot report on one good road as we speak right now. We want to thank the Governor for his speech, for the good work and the hopes that he is trying to give the people of Kilifi, but I think it is high time this hon. House to call the CECMs and explain to the House what they have been doing. Thank you so much, Mr. Speaker.

The Speaker (Hon.Mwambire): Hon. Members, in the exposition of the public policy contained in the Second Address by the Governor, we normally have four consecutive Sittings deliberating on the same. Let all the other Members who wish to speak now reserve their comments and they will be given an opportunity in the subsequent sittings.

ADJOURNMENT

The Speaker (Hon.Mwambire): There being no other business to transact, this House stands adjourned until 2:30 p.m. today.

The House rose at 11:41 a.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*